**SUMAIT University Journal (SUJ)**
eissn (2953-2698)
Issue No. 15 June 2024

# AINA ZA USIHIRI KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO

**Silima Faki Makame**
silimamakame3@gmail.com
School of Swahili and Foreign Languages
*Department of Swahili*
**Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA)**

*Received: April 2024, Accepted: junne 2024, Published June 2024*
*© SUMAIT University Journal 2024*

**Abstract:**

*This article investigates types of witchcraft in the **Dunia Uwanja wa Fujo** novel,(2007). The objective of investigating types of whitchcraft is to reveal the relationship existing between the Kiswahili literature and the culture found in the witchcraft. The data was collected from literature review of the selected novel. The selection of this novel originated from the preliminary information available with the researcher on the types of witchcraft reffered to in the novel. Data analysis was guided by the theory of Magic Realism. The findings of this article revealed that witchcraft is found in three main types: witchcraft which causes separation, witchcraft which brings unity and the witchcraft of deception. The three types confirm that literature is associated with the propagation of witchcraft and inversely witchcraft promotes literature in the process of the daily social life of Tanzanians.*

**Ikisiri***:*

*Makala haya yanachunguza aina za usihiri katika riwaya yaDunia Uwanja wa Fujo, (2007). Lengo la kuchambua aina za usihiri ni kudhihirisha na kuonesha uhusiano uliopo baina ya Fasihi ya Kiswahili na utamaduni kupitia aina hizo. Data za uchunguzi huu zilipatikana kwa njia ya uchambuzi wa maandiko katika riwaya teule. Kuteuliwa kwa riwaya hii kulitokana na taarifa za awali alizonazo mwandishi wa makala haya zinazohusu aina za usihiri katika riwaya hiyo. Uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Uhalisiaajabu. Makala haya yamebainisha kuwa aina hizo zinadhihirika katika namna tatu kuu. Mosi, usihiri wa kufarakanisha. Pili, usihiri wa kuunganisha. Tatu, usihiri wa kuhadaa. Aina hizo zinayakinisha kuwa fasihi ni kiambata kinachoutangaza usihiri na usihiri huwa chombo cha kuiendeleza fasihi katika mchakato wa maisha ya kila siku ya jamii ya Watanzania.*

**Keywords: Aina za Ushihiri Riwaya**

*E-mail:* silimamakame3@gmail.com

### *1.0 Utangulizi*

Neno usihiri lina asili ya Kiarabu liitwalo *sihiru* سحر limaanishalo *hadau* (hadaa) na kudanganya. Neno *sihiru* lilikopwa, likaingizwa katika lugha ya Kiswahili (*sihiri*)kwa kuwekewa kiambishi awali cha **u**, kubadilishwa irabu ya mwisho **u** hadi **i** na kuwa usihiri, kumaanisha uchawi (Abdulla, 1968, uk.106). Mlaga (2017,uk.7) anadai kwamba usihiri ni uwezo au nguvu ya kimiujiza yenye uwezo wa kuleta matokeo ya aina fulani, kulingana na makusudio ya mtumiaji wa nguvu hiyo. Makame (2016, uk.3) naye anaeleza kuwa usihiri ni uchawi wa maneno na matendo ya hadaa kupitia msaada wa jini na shetani ili kudhuru. Aidha, BAKIZA (2010, uk.369) linasisitiza kuwa usihiri ni uchawi unaodhuru kwa kukanyagwa au kuliwa. Hivyo, makala haya yameitazama dhana ya usihiri kuwa ni zao la utaalamu wa ushirikina ili kupata matokeo chanya au hasi kwa mujibu wa matakwa ya msihiri na muktadha lengwa kisihiri. Usihiri ni dhana pana iegemezwayo katika miegamo ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.Tafiti zilizotangulia zimechunguza kwa kisasi kidogo suala la usihiri katika fasihi ya Kiswahili. Watafiti kama vile,Safari (1993, kur. 154-160); Ali (2014, kur. 15-30), Makame (2016, kur. 114-140) na Mpalanzi (2016, uk.132). Tafiti zao zimelidokeza kwa jumla suala hilo kwa kuhusisha sababu na athari za usihiri bila ya kuweka bayana aina za usihirina mdhihiriko wake kwa mawanda mapana. Kutowekwa bayana kunasababisha uelewa mdogo wa wanajamii kuhusu usihiri. Pia, kunafinya mawanda ya uga wa fasihi, hususani riwaya ya Kiswahili. Mwanya huu uliibua chachu ya mtafiti kufanya utafiti ulioibua makala haya. Hivyo, makala haya yamelishughulikia suala la usihiri kwa mtazamo wa kifasihi. Kujiegemeza katika fasihi kunatokana na ukweli kwamba fasihi ni kiambata kinachoutangaza usihiri na usihiri huwa chombo cha kuiendeleza fasihi (Mulokozi, 2017, uk. 7;Mutembei, 2009, kur. 21-23; Ponera & Kikula, 2017, kur. 101-103)Aidha, huwa ni viwakilishi vya imani za kijadi, kuadabisha, kukomboa jamii na msingi wa kuwasilishia ukweli wa maisha ya wanadamu (Mlaga, 2017, uk.7). Hii inamaanisha kuwa fasihi na usihiri hubainisha falsafa ya Kiafrika, huhifadhi na kuonesha maarifa ya tiba asili.

Ufafanuzi huu unalenga kutoa mwanga kuwa fasihi inaakisi jamii na pia riwaya zinazokuwepo iliakisi vipengele vya uchawi kwa lengo la kukejeli mila na desturi zilizoenea nchini Tanzania wakati wa uandishi wake; kwani, huwakilisha mifumo ya kijamii ikiwamo ya kiutamaduni. Hii inadhihirisha kuwa fasihi ni kioo cha jamii; kwani, waandishi wa fasihi huwa hawaandiki katika ombwe. Msokile (1992, kur.94-96) anaeleza kuwa mwandishi anayebuni maandishi anapata mawazo yake kutoka katika mazingira yake yaliyomlea na kumkuza ama kumfinyanga kwa kila hali. Katika namna kama hiyo inadhihirika kwaEuphrase Kezilahabi katika riwaya ya*Dunia Uwanja wa Fujo*, (2007). Kwa hiyo, kitendo cha mwandishi kudhihirisha aina hizo, kilimsukuma mwandishi wa makala haya kuziweka bayana aina za usihiri kupitia riwaya teule. Kwa jumla, makala haya yamechambua aina za usihiri katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*.

## *2.0 Kiunzi cha Nadharia*

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Uhalisiaajabu; inayoweka bayana Mwenendo wa Uhalisiajabu. Msingi wa nadharia hii ulitumika katika mchakato mzima wa kukusanyia data, kuzichanganua na kuziwasilisha. Uhalisiaajabu uliasisiwa na Franz Roh mwaka 1925. Franz Roh aliitumia nadharia hiyo alipoifafanua picha iliyoonesha uhalisi uliopindwa kiajabuajabu ili kuonesha uhalisiaajabu uliomo pichani humo kisihiri (Walibora, 2010, uk. 143; Wamitila, 2003, uk. 274; Senkoro, 2007, kur. 1-3; Wafula, & Njogu, 2007, uk. 113;Faustine, 2017, kur.29-31).Uchambuzi wa makala haya umejiegemeza katika muhimili mmoja wa nadharia hii. Muhimili huo unabainisha kuwapo kwa nguvu za kisihiri zinazosababisha matokeo fulani ya aina za usihiri kulingana na makusudio ya mtumiaji wa nguvu hizo, kupatikana katika maisha halisi ya jamii na riwaya za Kiswahili duniani. Nguvu za kisihiri huelezwa kwa namna ya moja kwa moja inayofanya zionekane za kawaida kudhihiri katika jamii na riwaya hizo (Mbatiah, 2001, uk. 60; Mlaga, 2017, kur. 7-8; Wamitila, 2002, uk. 117 na 2003, uk. 274). Muhimili huu umetusaidia kuchambua aina za usihiri katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Aina hizo zimejadiliwa kwa mwegamo wa kifasihi kwa sababu fasihi ni kiambata kinachoutangaza usihiri na usihiri huwa chombo cha kuiendeleza fasihi (Mlaga, 2017, kur. 7-8; Mutembei, 2009, kur. 21-92; Ponera & Kikula, 2017, kur. 101-103; Ponera & Badru, 2019, uk. xx). Kwa hivyo, aina za usihiri zilizojadiliwa katika makala haya ni zile zilizosawiriwa na mwandishi katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, (2007). Aina hizo zimetuwezesha kupata picha halisi ya mdhihiriko wa usihiri uliosawiriwa katika riwaya hiyo.

## *3.0. Methodolojia*

Makala haya yaliongozwa na mkabala wakitaamuli katika kuzikusanya, kuzichunguza, kuzichuja na kuzichanganua data za utafiti uliozaa makala haya. Ponera (2019, uk.11) anasisitiza kuwa mkabala wa kitaamuli ni uchunguzi wa kina wa kisayansi ufanywao kwa kutafakari na kuchanganua jambo maalumu kwa lengo la kupata maarifa mapya au kuongeza ufahamu. Maelezo hayo yanaweka bayana kuwa mkabala huu ulitumia mbinu ya maelezo. Hii ni kwa sababu mkabala wa kitaamuli hauruhusu matumizi ya takwimu katika kutoa ufafanuzi na maelezo ya data zilizohusiana na utafiti uliofanyika. Hivyo, mkabala huu uliruhusu kutumika njia ya uchambuzi wamaandiko kupitia mkabala wa uhakiki wa kitamaduni katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, (2007). Data zilizopatikana kutokana na chanzo hicho zilikuwa mahususi kwa ajili ya kuugundua mdhihiriko wa usihiri kupitia aina za usihiri.

## *4.0 Aina za Usihiri Zinazojitokeza katika Riwaya Teule*

Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* inahusu falsafa ya udhanaishi uliojikita kuyaangalia maisha Kibwege kwa namna ya kisihiri kiajabuajabu. Waandishi wa mwelekeo huu wanaamini kwamba maisha hayana maana. Riwaya hii ni ya daraja la kwanza ya kijamii,

iliainishwa kuwa ni riwaya za uhalisia wa kihakiki na iliakisi vipengele vya uchawi kwa lengo la kukejeli mila na desturi zilizoenea nchini Tanzania wakati wa uandishi wake. Falsafa ya udhanaishi ilisaidia kugundulika kwa aina za usihiri unaoainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali. Miongoni mwavyo ni nyenzo zitumikazo kuuunda, matokeo au athari yake, pamoja na mchakato au matendo. Aina hizo zimepatikana kwa kutumia kigezo cha matokeo au athari za kisihiri. Utafiti uliozaa makala haya ulizingatia kuwa matokeo au athari zilizojiri baada ya kudhihiri kwa usihiri ndicho kilichoiainisha aina ya usihiri husika. Makala haya yalibaini kuwapo kwa aina za usihiri zilizogawika katika makundi matatu kupitia riwaya teule. Makundi hayo ni: Usihiri wa kufarakanisha, usihiri wa kuunganisha na usihiri wa kuhadaa. Ufafanuzi wa aina hizo ni huu ufuatao:

### *4.1 Usihiri wa Kufarakanisha*

Baali (1416H, kur. 104-105) anaeleza kuwa usihiri wa kufarakanisha ni uchawi wa kuingiza chuki, bughudha na mfarakano wa kisihiri kupitia jini au shetani. Usihiri huo hujiri baina ya mke na mume, mtu na mtu, mtu na wazazi, mtu na ndugu yake, mtu na rafiki au mshirika wake, mtu na ulimwengu hadi kufariki kimazingara. Hivyo, usihiri wa kufarakanisha ni uchawi wa kutenganisha na kuachanisha baina ya wasihiriwa walioshikamana kwa muda mrefu, au vitu wanavyovimiliki hadi kuwa mbali navyo, kupitia msada wa jini na shetani. Usihiri huo humfanya msihiriwa hujitenga na kila jambo au mtu bila ya kujitambua au kufariki dunia kisihiri.

Tukio la kwanza katika matukio yanayoudhihirisha usihiri wa kufarakanisha kupitia riwaya teule linahusu mbinu za kumtisha Tumaini[1] kimazingara. Mwandishi anaeleza:

> *Tumaini … alifurahi kuona kwamba wasichana walikuwa wakigombana na kupigana kwa ajili yake ... Wale wenye mabinti walianza kumchukia. Badala ya wazazi wa Leonila na Anastasia kugombana walifanya mkutano pamoja kufikiria njia ya kumkomesha Tumaini. Mulele alitaka Tumaini ahame kabisa kutoka kijijini. Kasala alitaka Tumaini amwoe Leonila kwa nguvu ... Siku chache zilizofuata, Tumaini alianza kuwa anasumbuliwa usiku. Siku moja alikuta mlango wa nyumba yake juu ya paa. Siku nyingine alitupiwa mchanga dirishani. Na ilikuwa hasa kumfanya Tumaini ahame. Tumaini angalihama upesi kama mambo fulani yasingalitokea. Mambo hayo yaliwafanya wenyeji wamsahau Tumaini kwa muda … Tumaini … Alianza kufikiri … watu wamekwishaanza kunikasirikia kwa kuharibu binti zao! … nitoroke niende nchi za mbali kabla mtumbwi haujatoboka …" Tumaini ... Siku chache … alikata shauri kutoka kijijini (kur. 26-32).*

Maelezo hayo yanaelezea mbinu kama vile vitisho vya kifo na uchawi dhidi ya msihiriwa zilizotumika kumhamisha na kumfarakanisha Tumaini na makazi yake,wapenzi wake,

[1]Ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mhusika huyo amesawiriwa kuyadhihirisha matendo ya kisihiri pamoja na kufanyiwa usihiri wa aina mbalimbali kupitia Mugala na Leonila.

pamoja na jamaa zake. Usihiri huo ulibainika kupitia nadharia ya uhalisiaajabu yenye muhimili unaoelezea kuwapo kwa nguvu za kisihiri zinazoudhihirisha kimazingara. Hii ni kulingana na makusudio ya wasihiri waliotumia nguvu hizo kumhamisha Tumaini kisihiri na kuudhihirisha usihiri huodhidi yake. Suala hilo lilifanikishwa na Mulele pamoja na wazee wenye mabinti waliomchukia, kumsihiri Tumaini kwa kumtisha usiku kisihiri. Vitisho hivyo vilifanikishwa kwa kuupachika mlango wa nyumba ya Tumaini juu ya paa la nyumba yake. Danah (2023, uk. 169) anasisitiza kuwa mtu mwenye tabia chafu zinazotia aibu katika jamii, mzinifu anayetembea na watoto wa watu, wake au waume wa watu, hufanyiwa usihiri wa kufarakanisha. Usihiri huo humtenganisha msihiriwa na watu anaoshirikiana nao, kuachana na tabia hizo, kumtia maradhi na kumhamisha katika mji bila msihiriwa kujijua. Usihiri huo huingizwa katika maji ya kunywa, kisha, hupewa msihiriwa anywe, huwekwa njia panda anayopita msihiriwa na jini na shetani huambatanishwa ili kuufanikisha usihiri huo. Msihiriwa hudhihirikiwa na mambo ya ajabuajabu yanayomtisha, humtia hofu na huachana na kufarakana na jambo alilolizoea kulifanya kimazingara kama ilivyojiri kwa Tumaini. Mtafiti anaona kuwa vitisho hivyo vilidhihiri kwa kuuweka mlango wa nyumba ya Tumaini juu ya paa lake kisihiri.

Katika tukio la pili, linahusu mdhihiriko wa dalili za usihiri wa kufarakanisha aliofanyiwa Muyango. Usihiri huo ulimfanya mhusika huyo atengane (afarakane) kisihiri dhidi ya familia yake na dunia (afariki). Mtunzi anaeleza:

> *Tumaini alipokuwa darasa la kumi na mbili mama yake aliugua na kuvimba. Madaktari walikuwa hawawezi kuuponya ugonjwa huu hata kwa kisu chao cha uchawi; kwani baada ya kupasua tumbo mgonjwa hupungukiwa sana na damu; hufa ganzi upande mmoja na hazungumzi tena mpaka kufa (uk. 14).*

Maelezo haya yanazisawiri dalili za usihiri wa kufarakanisha. Dalili hizo ni mgonjwa kuvimba tumbo, kupungukiwa na damu, hufa ganzi upande mmoja, kutozungumza mpaka kufariki. Dalili hizo hudhihiri kwa msihiriwa kurogwa kwa kulishwa mchanganyiko wa dawa za kienyeji. Usihiri huo ulibainika kupitia Nadharia ya Uhalisiaajabu yenye muhimili unaoelezea kuwapo kwa nguvu za kisihiri. Nguvu hizo huudhihirisha usihiri huo kulingana na makusudio ya wasihiri waliotumia nguvu hizo kuwasihiri wahusika hao. Utafiti uliofanyika kuyafanikisha makala haya uligundua kuwa mama yake Tumaini alisihiriwa kwa usihiri wa kufarakanisha uliomvimbisha tumbo kimazingara. Danah (2023, kur. 169-171) anashadidia kuwa miongoni mwa dalili za usihiri wa kufarakanisha ni kumwingiza maradhi msihiriwa yasiyotibika hospitali. Maradhi hayo husababisha kifo kwa msihiriwa, kufarakana na ulimwengu, jamaa na familia yake. Katika jamii ya Watanzania usihiri wa aina hii umeshika kasi; kwani, hudhihiri wasihiriwa wengi wanaoumwa na matumbo ya aina hii kimazingara.

Tukio la tatu linahusu mauaji ya kisihiri ambapo familia ya Tumaini ilisihiriwa hadi kuuliwa. Usihiri huo ulimvaa msihiriwa na kupata maradhi ya ajabuajabu hadi kufariki ukoo mzima wa Tumaini. Mtunzi anaeleza:

> *Lakini wakati huu mtu fulani alikuwa amekata shauri kumaliza ukoo wao wote. Tumaini alipoingia darasa la tisa baba yake alikufa … Muyango alikufa siku chache baadaye. Wakati wa mazishi … dada yake Muyango alikataa kulia … "Hamziki dada yangu," alisema. Watu walifikiri kwamba alimsahau kwa sababu ya ugonjwa wa tumbo ambao ulikuwa umekwisha kumdhoofisha. Baada ya kifo cha mama yake. Tumaini alikata shauri kuacha shule … Mugala alianza kucheka hali akizungumza peke yake … "Nimekwisha kata shauri kuumaliza ukoo wao. Na nitaumaliza (kur. 12-19).*

Dondoo hili linavisawiri vifo vya kimazingara vilivyowasibu wazazi wa Tumaini. Vifo hivyo huudhihirisha usihiri wa kufarakanisha ulioisibu familia nzima ya Tumaini. Usihiri huo ulibainika kupitia Nadharia ya Uhalisiaajabu yenye muhimili unaoelezea kuwapo kwa nguvu za kisihiri. Nguvu hizo ziliudhihirisha usihiri huo kulingana na makusudio ya Mugala aliyeiangamiza familia ya Tumaini kisihiri. Utafiti uliofanyika ulioibua makala haya uligundua kuwa wazazi wa Tumaini walisihiriwa kwa usihiri wa kufarakanisha na kufariki. Suleiman (2015, uk. 7) anashadidia kuwa usihiri wa kuua hufanikishwa kwa kuchanganya mtishamba wa *hanjari* na *faijali* na kulishwa msihiriwa kimazingara. Mtafiti anaona kuwa usihiri huo uliwasibu wazazi wa Tumaini waliofariki kiajabuajabu.Usihiri huo ulitengenezwa na Mugala dhidi ya familia hiyo. Usihiri huo uliwaua wazazi wa Tumaini na kumfarakanisha Tumaini na wazazi wake ili awe mbali nao.

### *4.2 Usihiri wa Kuunganisha*

Ali (2014, uk. 92) anaeleza kuwa usihiri wa kuunganisha ni kitendo cha kishirikina kinachompendezesha mwanamke kwa mumewe kisihiri kupitia msaada wa jini. Makame (2016, uk. 81) anaunga mkono kuwa usihiri wa kuunganisha ni usihiri wa kuipendezesha nafsi ya msihiriwaimpende msihiri kimapenzi kupitia msaada wa shetani na jini. Hata hivyo, mwandishi wa makala haya anaona kuwa usihiri wa aina hii hautekelezwi tu na mwanamke bali pia mwanamme kwa mwanamke. Aidha, usihiri huo hauelekezwi kwa mume tu bali hata kwa mwaname wa nje ya ndoa na mwanamke wa nje. Hivyo, usihiri wa kuunganisha ni uchawi wa limbwata anaofanyiwa msihiriwa wa kike au wa kiume ili kuipendezesha na kuipumbaza nafsi ya mmoja kati yao kimapenzi. Kenyatta (2004, uk.23) anashadidia kuwa usihiri wa kuunganisha ni dawa ya kisihiri inayoimarisha mapenzi, kuingiza upole na kuivutia haiba ya msihiri machoni mwa msihiriwa kimapenzi. Mtaalamu huyo anaendelea kuweka wazi kuwa usihiri huo huwekwa katika chakula, maji, vivywaji, kuchanjia mwilini mwa msihiri, kufukiza, kufukia ardhini, kutundika agani, kujipaka na kindorobi.

Tukio la kwanza linaloelezea usihiri wa kuunganisha unaofanikishwa na bibi (Mugala) mbele ya mjukuu (Leonila) wake. Usihiri huo ulilenga kumpumbaza kimapenzi Tumaini dhidi ya Leonila. Mtunzi anaeleza:

> *Mugala alipoona kwamba Leonila alipata mimba alianza kujuta kwa nini hakumchukua Tumaini zamani. Na alipoona kwamba Leonila alikuwa akimpenda sana rafiki yake, ile nia ya kumharibu Tumaini iliondoka kichwani mwake. Badala yake alianza kumpa Leonila dawa za mapenzi. Tumaini alipokuwa akiomba maji ya kunywa aliletewa maji yaliyokuwa yamechanganywa na dawa hizo. Tumaini bila kufahamu alikunywa (uk. 20).*

Dondoo hili linaelezea hoja ya msingi ya kuwapo kwa dawa zinazochanganywa na maji ili kuufanikisha usihiri wa kuunganisha kimapenzi. Usihiri huo ulibainika kupitia Nadharia ya Uhalisiaajabu yenye muhimili unaoelezea kuwapo kwa nguvu za kisihiri. Nguvu hizo huudhihirisha usihiri huo kulingana na makusudio ya wasihiri waliotumia nguvu hizo dhidi ya msihiriwa. Utafiti ulioyafanikisha makala haya uligundua kuwa Tumaini alisihiriwa usihiri wa kuunganisha kimapenzi. Uliofanywa na Mugala kwa kushirikiana na Leonila kupitia dawa zilizotiwa katika maji ya kunywa. Msali (2018, kur. 25-29) anashadidia kuwa msihiriwa huandikiwa talasimu ya mapenzi inayochanganywa na mtishamba wa mlazalaza, nguvu za jini, shetana na manuizi ya kumpumbaza na kumpendezesha msihiriwa kisihiri mbele ya msihiri. Mchanganyiko wa dawa hizo hutia ndani ya maji au chakula na hupewa msihiriwa. Nguvu za dawa hiyo humfanya msihiriwa ampende mke, mume, mwanamke au mwanamume bila ya kijitambua. Mtafiti anaona kuwa suala linalozingatiwa katika usihiri wa kuunganisha kimapenzi ni msihiri kumfanyia usihiri msihiriwa ili apendwe kupitia dawa ya mapenzi, nguvu za jini na za shetani.

Tukio la pili linalousawiri usihiri wa kuunganisha kimapenzi unaofanikishwa kwa kuwanasa wasihiriwa kimazingara.Wasihiriwa hao walipigwa makofi ya kimazingara usiku na hupatwa na bumbuazi linalowafanya wasitambue wanakokwenda. Mwandishi anaeleza:

> *Watu walikuwa hawajapata kufahamu mji wa Kasala sawasawa. Mji wa Kasala ulikuwa mgumu kufahamika kama pango la wezi, ambamo ukiingia hufahamu uendako. Kama ukiingia mji huu wakati wa usiku, utapigwa makofi na watu ambao huwaoni. Mapenzi; mapenzi ndiyo yalifanya mji wa Kasala ukafahamika baadaye. Mapenzi hayaogopi hatari yoyote. Mapenzi ndiyo yaliyowaleta vijana nyumbani kwa Kasala: Kasala alikuwa na binti wawili wazuri kupindukia. Ingawa mji wa Kasala uliwanasa vijana kama mtego wa buibui, Kasala na mke wake Mungere hawakuwa watu wa ajabu. Walikuwa watu wa kawaida na wema. Kasala na mke wake walikuwa wakiishi raha mstarehe (uk. 4).*

Dondoo hili linalisawiri zindiko la usihiri wa kuunganisha. Zindiko hilo huwapiga na kuwanasa wasihiriwa hao kimazingara na kuudhihirisha usihiri wa kuunganisha kimapenzi. Usihiri huo ulibainika kupitia Nadharia ya Uhalisiaajabu yenye muhimili unaoelezea kuwapo kwa nguvu za kisihiri. Nguvu hizo huudhihirisha usihiri huo kulingana na

makusudio ya Kasala aliyeweka zindiko hilo ili kuwanasa watu wanaoshiriki mapenzi na watoto wake. Utafiti uliozaa makala haya uligundua kuwapo kwa usihiri wa kuunganisha kimapenzi. Uliobainika kupitia wasihiriwa walionasa, kupigwa makofi na kutofahamu waendako kimazingara. Suala hilo lilijiri baada ya wasihiriwa hao kuingia katika mji wa Kasala kwa kupigwa na watu wasioonekana. Msali (2018, uk. 39) anasisitiza kuwa msihiri anayempiga na kumgandisha msihiriwa kimazingara huandika talasimu ya zindiko la mji.Talasimu hiyo msihiri huyo huiandika kwa wino mwekundu, huisomea *Barahatii* 21, huifunga na uvi au nyuki, huinuizia manuizi ya kumgandisha na kumkabidhi jini, shetani na mzimu. Kisha, huifukia au huitundika katikati ya mji wake kisihiri. Mtu anayeingia kwa lengo la kufanya mapenzi na watoto au mke wa msihiri aliyefanya zindiko hulo hupingwa na kuganda katika mji. Hii hutegemea manuizi ya msihiri aliyeweka zindiko la kisihiri.

Mtafiti anaona kuwa zindiko hilo liliwafanya wasihiriwa hao kughumiwa, kutojua wanakokwenda na kupigwa makofi kimazingara. Suala hilo liliudhihirisha usihiri wa kuunganisha dhidi ya wasihiriwa hao nyumbani kwa Kasala. Kenyatta (2004, kur. 23-24) anasisitiza kuwa lengo la usihiri huo ni kuulinda mji na familia hiyo kimapenzi kwa nguvu za kisihiri. Mtafiti anaona kuwa usihiri wa mapenzi umeenea sana katika jamii yaWatanzania kwani, baadhi ya mitaa wasihiriwa wanaotaka kufanya uharibifu wa kimapenzi katika familia mbalimbali huganda au husibiwa maradhi ya tego za kisihiri.
Tukio la tatu linamsawiri Dennis anayefanyiwa usihiri wa kuunganisha kupitia chakula na kinywaji anachopewa na Vera kisihiri. Mtunzi anafafanua:

> *Dennis alipomaliza kusoma barua hii aliiweka pembeni. Alikwenda kufungua sanduku la nguo lililotajwa ... Ndani ya sanduku hilo hilo alikuta barua nyingi kutoka kwa wapenzi wa Vera. Barua zingine zilikuwa zimeandikwa katika lugha ya Kiarabu. Barua hizi alizichukua na kuwapelekea watu waliokuwa wakifahamu Kiarabu. Dennis alishangaa barua hizo zilipofasiriwa. Barua mbili zilitaja dawa ya kuweka ndani ya chai ili kumfanya Dennis ampende sana Vera. Mbili zingine zilieleza dawa ya kuweka ndani ya chakula ili kumpumbaza D. akili asiwe na wivu. Barua hizi zote alizifunga vizuri na kumtumia Vera. Ilionekana wazi kwamba Mama Resi alikuwa amezoea kuwatembelea mashehe na lile buibui ndilo alikuwa amezoea kwenda nalo (kur. 110-111).*

Dondoo hili linafafanua kuwapo kwa barua zinazoelezea dawa za usihiri zinazowekwa katika chakula na kinywaji dhidi ya Dennis. Dawa hizo zinaudhihirisha usihiri wa kuunganisha kimazingara. Utafiti uliofanyika uligundua kuwa usihiri wa kuunganisha ulifanikishwa kupitia dawa ya mapenzi inayowekwa ndani ya chai na chakula. Hindawi (2003, kur. 99-100) anasisitiza kuwa usihiri wa kuunganisha ulifanikishwa na msihiri huyo kwa kupiga ramli iliyoitambulisha nyota ya msihiriwa. Pia, msihiri huyo alinuizia manuizi ya kumpumbaza msihiriwa kimapenzi na alimtuma jini na shetani waliompendezesha msihiriwa mbele ya msihiri.

Utafiti uliozaa makala haya uligundua kuwa Vera aliziingiza dawa hizo katika chakula na kinywaji kwa kunuizia kuwa nguvu za dawa hizo zimvae Dennis na asijitambue kimapenzi dhidi ya Vera. Jini aliyekabishiwa dawa hizo alimpumbaza Dennis kimapenzi na kuudhihirisha usihiri wa kuunganisha kimapenzi kupitia nguvu za jini, chakula na kunywaji kimazingara. Nguvu za usihiri zilisambaa katika damu na ziliiharibu mishipa ya fahamu ya Dennis. Mtafiti anaona kuwa jini huyo alimdhibiti Dennis ili ampende Vera mapenzi makubwa kupitia nguvu za kisihiri. Hatimaye, Dennis alidhihirikiwa na mandhari ya kumwona Vera kuwa na haiba ya kuvutia machoni mwake. Usihiri huo uliyahadaa macho ya Dennis kimapenzi mbele ya Vera. Jambo hilo lilichochea damu ya Dennis kuwa na mihemko ya kimapenzi dhidi ya Vera.Al-Hanbalii (1989, kur. 12-14) anasisitiza kuwa msihiriwa aliyesibiwa na usihiri wa kuunganisha hudhihirikiwa kuwa na mihemko hiyo. Iliyochangiwa na virutubisho vya kinywaji na chakula chenye dawa ya usihiri mwilini mwake. Masuala hayo yalitendeka kimwathiriano kupitia matakwa ya jini Mahaba, aliyeambatanishwa katika dawa za usihiri dhidi ya Dennis.Kupitia nguvu za kisihiri zilizoudhihirisha usihiri wa kuunganisha kimapenzi kiajabuajabu. Danah (2023, kur. 203-208) anasisitiza kuwa usihiri huo humfunga mdomo msihiriwa kisihiri ili asizungumze jambo lolote mbele ya msihiri.

Mtafiti anaona kuwa usihiri huo aliufanya Vera dhidi ya Dennis kwa kuweka dawa hizo ndani ya chakula na chai. Dawa hiyo aliitumia Vera kwenda kinyume na ndoa yake kwa kushiriki ngono-zembe kwa mwanamume anayemtamani kimapenzi. Hii inamaanisha kuwa Vera alijipatia pesa kwa kufanya ukahaba na kujiuza kingono kupitia dawa za usihiri wa kuunganisha kimapenzi. Ali (2014, uk. 92) anasisitiza kuwa msihiriwa aliyesibiwa na usihiri wa kuunganisha kimapenzi hufanyiwa jambo lolote baya bila ya kuwa na wivu mbele ya mke wake. Msihiriwa huyo hawezi kumkataza mke au mume wake asiende kinyume na ndoa yao. Pia, msihiriwa aliyelishwa dawa za usihiri humpenda msihiri aliyemsihiri mapenzi makubwa na kumtii kwa kila analolitaka kimapenzi. Masuala hayo yalibainika kupitia Vera aliyemsihiri Dennis hadi akawa mtumwa wa mapenzi kiajabuajabu kupitia nguvu za usihiri.

### *4.3 Usihiri wa Kuhadaa*

BAKITA (2015, uk. 371) linaeleza kuwa kuhadaa ni kitendo cha kumfanyia hila za udanganyifu mtu mwingine kwa lengo la kujinufaisha isivyo halali. Hoja hiyo inaweka bayana kuwapo kwa usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe. Makame (2016, uk. 85) anabainisha kwamba usihiri wa kuhadaa ni mazingaombwe yanayosimama juu ya matendo ya hadaa, ujanja na kudanganya kwa kutumia msaada wa shetani katika kuukamilisha kwake. Hivyo, usihiri wa kuhadaa ni uchawi wa mazingaombwe na kiinimacho kilichojengewa taswira ya hadaa ya uoni wa jicho lione kinyume cha uhakika wa mambo ulivyo mbele ya hadhira.

Aidha, Baali (1416H, kur. 87-85) na Kabwili (2016, kur. 35-42)wanaeleza kuwa usihiri wa kuhadaa ni uchawi wa mazingaombwe unaotawaliwa na sifa bainifu za kisihiri zifuatazo. Mosi, hadaa ya kisihiri hudhihiri mbele ya hadhira ya watazamaji kwa kuyazuga macho yao. Pili, baadhi ya wakati huwaogopesha watu kutokana na mdhihiriko wa ghafla machoni mwao kisihiri. Tatu, hufanikishwa kwa ufundi na ubunifu wa wasihiri unaokibadilisha kitu kisihiri. Nne, kitu huonekana kikitikisika na kutembea ingawa hakina uwezo huo. Pia, kitu chenye uwezo wa kutikisika na kutembea huzuiliwa kimazingara hadi kutulizana kabisa. Tano, huonwa jambo au umbile lililo dogo hukuzishwa na lililo kubwa hudogoshwa na kupunguzwa kimazingara. Sita, huonwa jambo au kitu katika mdhihiriko usio wa uhakika kwake. Al-Answar (2014, kur. 11-24), Mkama (2007, kur. 2-12) na Mshana (2006, uk. 13) wanaeleza kuwa sifa ya saba ya usihiri huo ni kuwapo kwa mandhari inayotawaliwa na undotondoto, nguvu za usihiri, kubadilika kimazingara kwa mtu au kitu na kuwapo kwa nguvu za ziada zinazofanikisha uzugaji na mazingaombwe. Nane, hutegemea mikanganyiko mingi ya uoni wa macho mbele ya hadhira. Tisa, kuwapo kwa uharaka na wepesi wa kuliunganisha jambo la kwanza ndani ya la pili kihadaa na kimazingaombwe. Hii huchangia kudhihiri kitu kingine kipya machoni mwa watazamaji wanaozugwa kimazingaombwe dhidi ya kile kilichokuwapo kabla. Usihiri wa kuhadaa uchawi wa udanganyifu unaotofautiana na aina mbili zilizopita kwa sababu: Hauhusiani na utamaduni wa jamii katika mila na desturi zake. Ni burudani tu kwenye sherehe, na jukwaa la kuonyesha uchawi huu wa bandia mbele ya hadhira ya watu wazima na watoto. Kwa kuongeza, uchawi huu haudhuru mtu yeyote katika watazamaji

Ufafanuzi huo unathibitisha kuwapo kwa usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe kupitia riwaya teule.

Tukio la kwanza linausawiri usihiri wa kuhadaa unaojiri mbele ya hadhira iliyoshangazwa na mazingaombwe hayo. Mwandishi anaeleza:

> *Katika kundi la Muganga Golita jitu kubwa lilipandishwa juu. Lilikuwa na sura ya ng'ombe. Ndani ya jitu alikuwa amewekwa mtu. Mtu huyu alikuwa haonekani. Akiwa mle ndani alivuta kamba za midomo ya mbele ya lile jitu kwa vile kwamba lilionekana kutafuna majani yaliyokuwa yamelijaa mdomoni. "A! A! Linakula!" Anastasia alimsukuma Tumaini. Tumaini alikuwa amenyamaza. "Linacheka hata kucheka. Linajipangusa jasho! Angalia!" Tumaini alikuwa amenyamaza. Alikuwa amekufa mzima. "Tazama yule mtu! John alisema, "anatema moto kutoka mdomoni!" Katika kundi la Funga Bilima mtu alizikwa chini udongoni, na moto ulikuwa palepale alipozikwa. Watu wengi walingojea kuona nini kitatokea. Baada ya nusu saa walichimba kumtoa. Alikuwa mzima! Katika kundi hili hili kulikuwa na mtu aliyekuwa amechukua pipa la maji kwa mikono miwili. Kwa jumla viini-macho vingi sana vilifanywa. Labda hata mambo ya uchawi, maana mengi yalikuwa hayaaminiki (kur. 51-52).*

Hoja ya msingi inayobainika katika nukuu hii ni kuwapo kwa mbinu za kuudhihirisha usihiri wa kuhadaa uliobainika kupitia mambo yafuatayo: Mosi, kuwapo kwa jitu lililoingizwa mtu lenye sura ya ng'ombe lililopandishwa juu katika kundi la Muganga Golita. Utafiti uliozaa makala haya uligundua kuwa Jitu lilipandishwa juu na kuingizwa mtu wa kimazingara ni taswira ya jini. Jini huyo aliudhihirisha usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe kwenye kundi la Muganga Golita.Hindawi (2003, uk. 107) anasisitiza kuwa usihiri wa kuhadaa ni mazingaombwe yanayofanikishwa na msihiri kwa kuingiza kitu ndani ya kitu au mtu katika taswira ya mtu mwingine kiumithilisho. Mambo hayo hujiri kinyume na uhakika wa mambo yanayojiri katika maisha ya kawaida ya wanadamu. Naye, Swanaibu (2014, uk. 26) anaona kuwa anapodhihirika mtu aliyesawiriwa ndani ya mwingine huwa ni dalili ya kuudhihirisha usihiri wa kuhadaa kimazingaomwe unaoyahadaa macho ya hadhira kisihiri.

Hussein (2011, uk. 11) anasisitiza kuwa jini wana uwezo wa kujibadilisha na kuwa na sura ya mnyama, mtu, ndege na kinyago kwa mujibu wa matakwa ya msihiri. Mtafiti anaona kuwa masuala hayo yaliudhihirisha usihiri wa hadaa kimazingaombwe katika kundi la Muganga Golita.

Makala haya yaligundua kuwa upo uhusiano baina ya kiongozi wa kundhi hilo, jini, shetani na mzimu. Vijenzi hivyo viliudhihirisha usihiri wa kuhadaa kupitia maelekezo ya kiongozi wa kundi la Muganga Golita dhidi ya hadhira iliyoshuhudia hadaa ya mazingaombwe hayo. Msali (2018, kur. 6-7) na Suleiman (2015, kur.6-10) wanasisitiza kuwa kuhadaa kupitia mazingaombwe hufanikishwa kwa dawa za usihiri. Dawa hizo hutengenezwa kwa mbaazi, mti wa *hanjari*, *faijali*, kifauongo, mafuta ya msukule na talasimu ya kujificha kimazingara mbele ya watu wanaofanyiwa mazingaombwe husika.

Makala haya yaligundua kuwa jitu lililoonekana na watazamaji katika kundi hilo lililokuwa juu ya pipa ni jini na shetani. Viumbe hao walidhihirishwa kupitia nguvu za usihiri mbele ya hadhira hiyo na kuudhihirisha usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe katika kundi hilo. Viumbe hao walijimithilisha na wanadamu ili kuyafanikisha mazingaombwe hayo kwa mujibu wa matakwa ya kundi la Muganga Golita. Suala hilo lilifanikishwa kupitia ishara iliyoyadhihirisha kimazingaombwe hayo kupitia mzimu, jini na shetani waliohudhurishwa na wasihiri mbele ya hadhira. Shar-qawi (1992, uk.70) anasisitiza kuwa usihiri wa kuhadaa hufanikishwa kwa hadaa na ujanja wa kiinimacho zinazomsibu msihiriwa. Msingi wa usihiri huo ni kulishughulisha jicho lione jambo linajiri kinyume na uhakika wake kupitia jini na shetani wanaoufanikisha usihiri huo au ujuzi wa mchawi na matumizi ya teknolojia ya kisasa na udanganyifu wa macho kimazingara.

Mtafiti anaona kuwa watu hao waliudhihirisha usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe mbele ya hadhira kupitia maelekezo ya kiongozi wa kundi la Muganga Golita kisihiri. Kiongozi huyo alimwamrisha jini aingiye ndani ya taswira ya jitu hilo na kudhihiri mbele ya hadhira hiyo. Jitu hilo lilikuwa jini aliyejenga taswira ya kivuli cha mtu ndani yake kimazingara.

Viumbe hao walidhihirishwa kwa mwonekano wa kiumbe mmoja aonekanaye ndani ya mwingine kupitia nguvu za kisihiri. Nguvu hizo huudhihirisha usihiri wa kuhadaa kiajabuajabu kwa kuvuta kamba na kutafuna majani mdomoni mwake kimazingara. Masuala hayo yalimshangaza Tumaini kutokana na kujiri kwake kimazingara mbele ya hadhira hiyo kupitia nguvu za kisihiri. Muhunzi (2015, kur. 34-36) anaona kuwa watu hao ni dalili zinazoudhihirisha usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe kama ilivyojiri kupitia kundi la Funga Bilima kiajabuajabu.

**Pili**, kuwapo kwa mtu aliyezikwa chini ardhini ni kwa kuwapo udongo na mtu aliyemithilishwa kupitia nguvu za kisihiri. Udogo huo ulitokana na mshabihiano wa udongo wa kisihiri na mtu huyo katika kundi la Muganga Golita. Mkama (2007, kur. 22-28) anasisitiza kuwa mdhihiriko wa miili na taswira za viumbe hao huwa za jini, wanaojidhihirisha kwa umbo la wanadamu ili kuudhihirisha usihiri wa kuhadaa. Pia, jini huyo hujidhihirisha mbele ya mwanadamu ili kumtisha, kumtia hofu, wasiwasi na kuyafanikisha mazingaombwe hayo mbele ya hadhira. Kupitia taswira ya kumfunika mtu aliyezikwa ardhini kimazingara. Pia, moto uliowekwa alipozikwa mtu wa kimazingara uliudhihirisha usihiri wa kuhadaa. Msali (2018, kur.13-19) anasisitiza kuwa moto unaowaka au unaowashwa ni wa kimazingara ulishabihishwa na moto halisi kuifanikisha hadaa ya kimazingaombwe mbele ya hadhira. Hii ni kutokana na jini na shetani waliotumwa na kiongozi wa kundi la Muganga Golita kuidhihirisha hadaa ya kimazingaombwe mbele ya hadhira. Viumbe hao hujisawiri wakitoa moto unaowaka kimazingara katika sehemu inayooneshwa mazingaombwe kupitia nguvu za kisihiri. Hii inamaanisha kuwa usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe ulitumika kuyahadaa macho ya wasihiriwa waliouona moto wa kimazingaombwe. Mtafiti anaona kuwa hadaa ya kimazingaombwe ilifanikishwa na msihiri kufukiwa shimoni akiwa hai na kufukuliwa akiwa mzima. Pia, kuwashwa moto wa mazingara juu ya shimo hilo kulifanikishwa kupitia taswira ya vivuli vya jini na shetani kisihiri.

**Tatu**, kuwapo kwa mtu aliyechukua pipa la maji kwa mikono miwili katika kundi hilo ni usihiri wa kuhadaa. Muhunzi (2015, kur. 39-41) anasisitiza kuwa suala hilo lilifanywa na jini na shetani kisihiri; kwani, linapotokea jambo lisilo la kawaida kufanywa na mwanadamu huwa ni hadaa za kisihiri. Viumbe hao hufanya viini-macho vinavyoifanya hadhira iamini kujiri kwa jambo hilo na kuudhihirisha usihiri wa kuhaa kama ulivyojiri katika kundi la Muganga Golita. Kupitia jitu lililotema moto na kuchukua pipa la maji kwa mikono miwili. Ali (2014, uk. 98) anashadidia kuwa masuala hayo huudhihirisha usihiri wa kuhadaa unaofanikishwa kwa kuvibadilisha vitu kimazingara kwa mujibu wa matakwa ya wasihiri wa kundi hilo. Katika jamii ya Watanzania usihiri wa kuhadaa kimazingaombwe kama huo hujiri kwenye maonesho ya bidhaa au kwenye sherehe za kiserikali na za watu binafsi.

Tukio la pili miongoni mwa matukio yanayoudhihirisha usihiri wa kuhadaa linamsawiri simba aliyeyadhihirisha hadaa ya kimazingaombwe mbele ya nyani. Tunaambiwa:

> *Siku moja simba na nyani walikuwa wakisafiri pamoja ... Njiani simba alimwambia nyani akaze mwendo … Wakabishana kwa muda mrefu. Matokeo ya ubishi huu ikawa ni kufanya mashindano ya mbio. Wakajipanga mstarini. Saa tatu zilipotimia simba alichomoka. Dume hilo! Mkia juu, manyoya kasambaza. Nyani mwendo wake ule ule, akawa anakula vumbi. Hakufika mbali alipoona kitu fulani kimeenea damu kikitembea kinyumenyume. Ajabu! Nyani alishangaa. Kile kitu ni kitu gani! Kile kitu kilimwambia nyani; Nyani! Ebu nitazame! Nyani alimwona simba amechunwa ngozi yake, damu inamvuja ovyo. Nyani alimwambia simba; rafiki, ebu nieleze yaliyokupata! Simba alitikisa kichwa chake kwa huzuni. Nyani alielewa. Alimwambia simba: rafiki, njia uliyopita ni mbaya, mimi sitaifuata … Simba alianguka chini akafa (kur. 77-78).*

Nukuu hii inalisawiri dume la simba lililotimka mbio mkia juu na kuchuruzika damu baada ya kuchunwa ngozi kimazingara. Pia, dume hilo lilitembea kinyumenyume. Usawiri huo unaudhihirisha usihiri wa kuhadaa. Usihiri huo ulibainika kupitia Nadharia ya Uhalisiaajabu yenye muhimili unaoelezea kuwapo kwa nguvu za kisihiri. Nguvu hizo huudhihirisha usihiri wa kuhadaa kulingana na makusudio ya simba aliyetumia nguvu hizo kujieneza damu ya kimazingara na kutembea kinyumenyume kisihiri. Kutokana na damu iliyoenea mwilini mwa simba, nyani alishangaa na kumwonea huzuni simba na kuifanikisha hadaa kimazingaombwe mbele ya nyani. Msali (2018, uk. 13) anaona kuwa usawiri kama huo hulenga kufanikisha hadaa ya msihiri kwa msihiriwa kisihiri. Simba alimhadaa nyani ili kutia hofu kwa nyani. Damu hiyo na mbio alizokimbia simba zilimithilishwa kisihiri kupitia jini na shetani waliojimithilisha kwa maumbile hayo. Hata hivyo, Swanaib (2014, uk.26) anaona kuwa dalili zilizodhihirika kupitia simba huyo zinaudhihirisha usihiri wa kuhadaa mbele ya hadhira hiyo. Hadaa hiyo ilifanikishwa kwa kuyahadaa macho ya hadhira na taswira za kimazingara. Mtafiti anaona kuwa masuala hayo yameenea katika jamii ya Watanzania na huufanikisha usihiri wa kuhadaa katika maisha ya kila siku.

### *5.0 Hitimisho*

Makala haya yalibainisha aina za usihiri zilizojitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Makala yamebainisha aina tatu kuu za usihiri zinazosawiriwa katika riwaya hiyo. Mosi, usihiri wa kufarakanisha. Pili, usihiri kuunganisha. Tatu, usihiri wa kuhadaa. Aina za usihiri wa kufarakanisha zilijumuisha mbinu za kumtisha Tumaini kimazingara, kudhihiri vifo vya kimazingara vinavyoudhihirisha usihiri wa kufarakanisha na kuwapo dalili za usihiri wa kufarakanisha aliofanyiwa Muyango. Usihiri wa kuunganisha ulihusisha mapenzi ya wanandoa na yasiyokuwa ya wanandoa.Kwa upande wa usihiri wa kuhadaa unahusiana na mazingaombwe yanaojiri mbele ya hadhira na simba aliyeyadhihirisha mazingaombwe mbele ya nyani. Aina hizo zinayakinisha kuwa fasihi na usihiri huhusiana katika maisha ya kila siku.

## MAREJELEO


- Abdahu, S. S. A. (2011), *Usuli-Sihiri*, Daru-Ibni-Jauzii, Kairo.
- Abdalla, M. S. (1968), *Kisima cha Giningi*, Nairobi Evans Brothers, Nairobi.
- Ali, U. M. (2014), *Upanga Mkali wa Kupambana na Wachawi Waovu,* Maktabatul-Qaswa, Dar es Salam.
- Al-Answari, A. A. M. (2014), *Min-Haji Salafi Fi-Ilaajil-Massi wa Sihiri*, Muasasatu Zadul-Maarifi, Kairo.
- اَلأنصار، ع .ع .م - 2014 منهج السَّلفِ في علآج المس وسحر،مـءسسة زيدُالمعارف،القاهرة
- Al-Hanbalii, A. M (1989), Ilajul -Umuri-Sihiriatu Mina Shariiatil-Islamiyati, Daru Ammar,
  - الهمبَلِيْ،ع. م . 1989 عيلآجُ الؤُمورسحرة من شريعة الإِسلآمية، دارُ عمَّار
- Baali, W. A. (1416H), Al-*Swarimul-Batari-Fi-Taswadi-Lisaharatil-Ash'rari*, Kutub Khana Islamiyat-ul-Islam, New-Delhi.
  - بعلي و. ع.1441 الصارم البتار في تصدي لسحرةالشرر،كتب خانّ الأسلآمية ا لإِسلآم، نودلح
- BAKITA, (2015), *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Longhom Publishers Ltd, Dar-es-Salaam.
- BAKIZA, (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press, Dar-es-Salaam.
- Chimerah, R. & Njogu, K. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Danah, A.A. M. (2023), *Hazina ya Tiba Ruhaniya*, Abunanal C. E. Press, Dar-es-Salaam.
- Faustine, S. (2017), *Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili,*Tasinifuya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.www.Journals.udsm,http://repository.costech.or.tz/handle/20.500.12661/2421URI:http://hdl.handle.net/20.500.12661/2421
- Hindawi, A. A. (2003), *Ilaju Sihiri,Wal-Massi Wal-Insi Wal-Jaani*, Maktabatu Tanaim, Kairo.
  - هندوي، ع.ع. 2003 علآجُ سحر والماس والأنسُ والجان ، مكتبة تناءم، القاهرة
- Hussein, S.S. (2011), *Yajue Majini*, Para Print Technology, Dar-es-Salaam.
- Kabwili, A. A. Y. R. (2016), *Utangulizi wa Migogoro ya katika Maisha ya Ndoa*, Mwandishi.
  - Kenyatta, P. A. (2004), *Imani ya Wamatego juu ya Uchawi, Kifo, Kindorobi na Ugangawa Kienyeji,* Peramiho Printing Press, Dar-es-Salaamu.
- Kezilahabi, E. (2007), *Dunia Uwanja wa Fujo*, Acme Press Kenya Ltd, Nairobi.
- Makame, S. M. (2016), *Matumizi ya Falsafa ya Usihiri katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi,* Tasnifu yaShahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.(Haijachapishwa).

- Mbatiah, M. (2001), *Kamusi ya fasihi*, Standard Textbooks Graphics & Publishers, Dar-es-Salaam.
- Mkama, S. Kh. (2007), Ulimwengu wa Majini na Vituko Vyao, Kara Stationary, Dar-es-Salaam.
- Mlaga, W. K. (2017), *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*, Heko Publishers, Dar-es-Salaam.
- Mpalanzi, L (2016), Mpaka kati ya Uganga na Uchawi: Uchunguzi Kutoka Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili Mirathi ya Hatari. *Udsm Journal*, 20(4), 130-150,https://journals.udsm.ac.tz.
- Mshana, A. A. M. (2006), *Utambuzi Juu ya Uchawi, Majini ,Husda na Tiba ya Habbat Saudaa*, Abuu Awadhi Stationary, Kagera Mikoroshini.
- Msali, H. F. (2018), *Elimu ya Tiba*, (Aka Babu), Mtunzi.
- Msokile, M. (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi,* Dar es Salaam University Press, Dar-es-Salaam.
- Mulokozi, M. M (2017), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu,*KAUTU, Dar es Salaam.
- Mutembei, A. K. (2009), *Ukimwi katika Fasihi ya Kiswahili*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Dar-es-Salaam.
- Muhunzi, B. Kh. (2015), Uchawi na Husda katika Qur-an na Sunnah, Kauthar Priners, Dar-es-Salaam.
- Ponera, A. S. & Kikula, I. S. (2017), *Misemo ya Vyambo vya Usafiri*, Afroplus Industries Limited, Dar-es-Salaam.
- Ponera, A. S. (2019), *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu,* Central Tanganyika Prees.
- Ponera, A. S. & Badru, Z. A. (2019), Koja la Taaluma za Insia kwa Heshima ya Profesa Joshua madumulla, xiv-xxv, Ponera, A. S. & Badru, Z. A. Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Roh, F. (1925), *Nach-Expressionismus-Magischer-Realismus*, Krinkhardt & Biermann Press, https:// www. Woridcat.org.
- Safari, A. J. (1993), *Fasihi,* Uandishi na Uchapishaji: Hisia katika Fasihi Andishi, *Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania*, 133-140. M. M. Mulokozi na C.G. Mung'ong'o, Dar es Salaam University Press.
- Senkoro, F. E. M. K. (2007), Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe. *Kioo cha Lugha*, Tol. 5, (uk. 1 - 12), Dar-es-Salaam.
- Shar-qawi, R. (1992), *Al-Ilajubil-Qur-an: Minal-Amradhil-Jaani*, Maktabatul- imani, Kairo.
- شرقوي، ر. 1992 العلاَجُ بالقرآن: من الأمراضِ الجان، مكتبة الأيمان، القاهر.

- Suleiman, Kh. (2015), *Ulimwengu wa Wachawi na Balaa Zao,* Kutub Khan Ishaatul-Islam, Dar-es-Salaam.
- Swanaib, GH. A. (2014),*SihiruWal-kuhanat: Al-jaanu walmalaikat,* Daru- Almaarifi Al-Azhari, Kairo.

  صنب ،غ .ع.2014 سحرُ والكهانة: الجان والملآـءكة، دارُالمعارفِ الأزهر، القاهرة.
- Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Sai Industries, Nairobi.
- Walibora, K. (2010), *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Swahili Forum 17 (2010) p.143-157.
- Wamitila, K. W. (2003), *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.*Focus Books, Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*, Phoenix Publication, Nairobi.